TAASISI YA UTAFITI
WA KILIMO TANZANIA

TARI



WADUDU WAHARIBIFU WA MINAZI,

ATHARI ZAKE NA UDHIBITI


Utangulizi

Mashambulizi ya wadudu: chonga, utitiri na mbu wa minazi husababisha minazi kukauka, udumavu na kudondoka kwa vidaka kwa kiwango kikubwa hivyo kupelekea uzalishaji wa nazi nchini kupungua kwa zaidi ya 50%.

WADUDU WAHARIBIFU WA MINAZI NA ATHARI ZAKE

1.CHONGA

Chonga ni jamii ya mbawa kavu, mwenye rangi ya kahawia na mbawa ngumu ya kuteleza. Hujulikana kama seremala kutokana na tabia yake ya kupekecha, kutoboa na kutoa vumbi vumbi kwenye minazi.



Picha 1(a) Mdudu chonga (b) athari za chonga kwenye majani ya mnazi


- ✓ Chonga hushambulia mnazi katika hatua zote za ukuaji na kusababisha madhara kwa mmea na mavuno yake.
- ✓ Huathiri zaidi minazi mikinda chini ya miaka 5, mashambulizi yakizidi mnazi hufa
- ✓ Chonga asipodhibitiwa hushambulia hadi minazi inayozaa na kusambaa kwenye minazi mingine

2. UTITIRI WA MINAZI

- ✓ Utitiri wa minazi ni mdudu mdogo sana mwenye umbo la minyoo
- ✓ Hushambulia vidaka vya umri wa miezi 2-5 kwa kupitia chini ya vifuniko vya vidaka hivyo

Dalili na athari za Utitiri kwenye Minazi

- ✓ Baka jeupe chini ya kifuniko cha kidaka ambalo huongezeka na kuwa rangi ya kahawia
- ✓ Sehemu iliyoshambuliwa huwa kovu gumu lizualo nazi kutanuka na hatimaye kuwa ndogo ndogo (Picha 2b)
- ✓ Nazi iliyoshambuliwa huwa na ganda gumu, ndogo na yenye ujazo mdogo wa mbata.



Picha 2(a) Utitiri wa minazi (b) athari za utitiri kwenye nazi

3. MBU WA MINAZI


- ✓ Mbu wa minazi ni wadudu wenye mchanganyiko wa rangi ya udongo na nyekundu na urefu wa milimita 14-15.
- ✓ Hutoa harufu kali waguswapo.
- ✓ Hufanana na wadudu aina ya kangambili wa zao la pamba na sufi.

- ✓ Hushambulia zaidi vidaka na nazi changa kwa kufyonza utomvu, kupoteza maji, kunyauka na hatimaye vidaka kudondoka

Udhibiti wa Wadudu waharibifu wa minazi

Mdudu Chonga


- ✓ Haribu mazalia ya chonga kwa kupasua magogo ya minazi iliyoathirika shambani (Picha 3a)
- ✓ Tumia ndoano maalum kutoa Chonga kwenye minazi mikinda
- ✓ Tumia mitego iitwayo "Rhinolua", yenye harufu iwavutiayo chonga, na kusababisha watumbukie ndani ya mtego (Picha 3b)
- ✓ Chonga waliotumbukia ndani ya mtego huangamizwa. Inashauriwa mitego mitano (5) kwa hekta moja. Mitego iwekwe katika kila pembe ya shamba na mmoja katikati. Njia hii hufanikiwa sana endapo wakulima wote wa eneo husika wataitumia.



Picha 3(a) Sondo ndani ya kigogo cha mnazi kilichooza na kupasuliwa (b) Mtego wa Rinolua

4. Mbu wa Minazi

- ✓ Dhibiti kwa kutumia wadudu rafiki (majimoto) wapatikanao kwenye mazao ya miti aina ya michungwa, mikorosho na miembe Hiivyo, inashauriwa shamba la minazi lichanganywe na mazao hayo



Picha 4(a) Mbu wa minazi na (b) Mashambulizi ya Mbu wa Minazi kwenye vidaka



Picha 6. Wadudu rafiki majimoto kwenye michungwa hushambulia mbu wa minazi

- ✓ Shamba liwe safi kwa ondoa magugu na vichaka vinavyohifadhi mazalia mbu wa minazi
- ✓ Tumia viuatilifu mzunguko (systemic insecticides)) kwenye minazi mikinda ili kudhibiti mashambulizi, au viuatilifu asilia vitokanavyo na mmea wa muarobaini vyaweza kutumika kwa kunyunyuzia kuzunguka shina au kupulizia kwenye vidaka.

UMUHIMU WA KUDHIBITI WADUDU WA ZAO LA MNAZI

- ✓ Udhibiti wa wadudu waharibifu ni muhimu kwa wakulima wa minazi ili kuongeza tija "zingatia kanuni bora za kilimo cha minazi na ushauri wa wataalamu"

Kwa ushauri wasiliana na Meneja

Kituo cha Utafiti wa Kilimo Mikocheni

+255 (0) 22 2700552

+255 (0) 676692467

Barabara ya Coca Cola,

Kitalu Na.22, Dar es Salaam,


Barua pepe: cmmikocheni@tari.go.tz

- Hushambulia zaidi vidaka na nazi changa kwa kufyonza utomvu, kupoteza maji, kunyauka na hatimaye vidaka kudondoka

Udhibiti wa Wadudu waharibifu wa minazi

Mdudu Chonga

- Haribu mazalia ya chonga kwa kupasua magogo ya minazi iliyoathirika shambani (Picha 3a)
- Tumia ndoano maalum kutoa Chonga kwenye minazi mikinda
- Tumia mitego iitwayo "Rhinolua", yenye harufu iwavutiayo chonga, na kusababisha watumbukie ndani ya mtego (Picha 3b)
- Chonga waliotumbukia ndani ya mtego huangamizwa. Inashauriwa mitego mitano (5) kwa hekta moja. Mitego iwekwe katika kila pembe ya shamba na mmoja katikati. Njia hii hufanikiwa sana endapo wakulima wote wa eneo husika watailtumia.



Picha 3(a) Sondo ndani ya kigogo cha mnazi kilichooza na kupasuliwa (b) Mtego wa Rinolua